East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004) na *Kifo Kisimani* (2001)

*Minyade Sheril Mugaduka[1*] & Jessee Murithi[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0001-6902-1895; Barua pepe ya mawasiliano: minyadesheril@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Itikadi, Propaganda, Usemi, Utamaduni, Uchanganuzi Tahakiki Usemi.*

**IKISIRI**

Itikadi ni fikra zote za maoni ya wanadamu kuhusu wanayoyasema na wanayoyafikiria kuhusu dini, sheria siasa, maadili na falsafa kama wanavyotaja Marx na Engels (1977). Propaganda hushawishi fikra za mtu kutenda jambo kwa namna fulani. Ni ushawishi unaoratibiwa kwa malengo fiche (Ellul, 1965). Tafiti zimefanywa katika kipengele cha itikadi. Murithi (2017) ametafitia itikadi katika riwaya za Said A. Mohamed; amechunguza itikadi katika riwaya teule kwa kuangazia maudhui, dhamira, wahusika mtindo na usemaji katika vipindi tofauti. Suala la itikadi pia limeshughulikiwa na Kitto (2019) ambaye ameonyesha ufungamano kati ya siasa na itikadi. Katika kipengele cha propaganda, Mlaga (2020) ameangazia uhusiano kati ya propaganda na fasihi. Ameonyesha mikakati na mbinu za kubainisha propaganda katika kazi za fasihi kwa kuegemea tungo teule za Muyaka, Mnyapala na Kezilahabi. Wahakiki wanachukulia propaganda na itikadi kama dhana moja. Utafiti haujafanywa unaobainisha itikadi na propaganda katika tamthilia za Kiswahili. Makala haya yanalenga kubainisha uhusiano uliopo kati ya itikadi na propaganda katika tamthilia za *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) na *Kifo Kisimani* (2001). Makala yataonyesha kuwa hizi ni dhana mbili tofauti lakini zina uhusiano. Utafiti umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi (UTU) ilioasisiwa na Norman Fairclough (1989). Ni nadharia ambayo hueleza uhusiano uliopo kati ya matukio ya kiusemi, kisiasa, kimatini, kijamii na kiutamaduni yanavyoathiriwa na itikadi. Huangazia jinsi usemi huo huathiri matukio katika jamii

**APA CITATION**

Mugaduka, M. S. & Murithi, J. (2022). Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) na Kifo Kisimani (2001). *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 110-123. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

**CHICAGO CITATION**

Mugaduka, Minyade Sheril and Jessee Murithi. 2022. “Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) na Kifo Kisimani (2001)”. *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 110-123. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004.

**HARVARD CITATION**

Mugaduka, M. S. & Murithi, J. (2022) “Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) na Kifo Kisimani (2001)”, *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 110-123. doi: 10.37284/jammk.5.2.1004.

**IEEE CITATION**

M. S. Mugaduka & J. Murithi “Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) na Kifo Kisimani (2001)”, *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 110-123, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Mugaduka, Minyade Sheril & Jessee Murithi. “Ufungamano wa Itikadi na Propaganda katika Tamthilia za Maua Kwenye Jua la Asubuhi (2004) na Kifo Kisimani (2001)”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 110-123, doi:10.37284/jammk.5.2.1004.

## UTANGULIZI

Dhana ya itikadi ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Destutt de Tracy mwisho wa karne ya kumi na nane na kukuzwa kikamilifu katika karne ya kumi na tisa (Larrain, 1979). Tracy alibaini itikadi kwa maana ya ‘sayansi ya mawazo’. Itikadi ni dhana iliyo na fasili nyingi. Ni dhana inayojumuisha maoni na fikra za wanadamu kuhusu wanayoyasema na wanayoyafikiria kwa kujikita katika vigezo vya kisheria, kidini, kisiasa, kimaadili na kifalsafa (Marx & Engels, 1977). Mamlaka ya itikadi yanatokana na uhalali bila kutumia nguvu. Kwa mujibu wa Gramsci (1971), ni ikibali ya hari. Marx na Engels (1977), wanaeleza itikadi kama maoni na fikra za wanadamu zinazohusisha mambo wanayoyasema na kuyafikiria kuhusu masuala ya kidini, kisheria, kisiasa, kiuchumi na kimaadili. Kwa mujibu wa Dijk (1998), itikadi huhusisha imani katika jamii kuhusu hali ya maisha inayojidhihirisha katika makundi ya kisiasa. Anaendelea kueleza kuwa itikadi hupitia mabadiliko katika historia. Baadhi ya imani za kijamii ni pamoja na haki za binadamu, usawa wa kijinsia miongoni mwa imani nyingine. Itikadi inaweza kusambazwa kupitia kwa maandishi au mazungumzo.

Propaganda hushawishi mtu ili afikirie na kutenda kwa namna fulani inayotakiwa. Imani huwekwa ili kushawishi vipengele vya ishara fulani. Hushawishi tabia za watu kwa malengo fiche. Prantkanis na Aronson (2001), wanaeleza kuwa propaganda ni mbinu ya kushawishi umma katika jamii ya kisasa. Ni dhana iliyoibuka na kutumika mnamo mwaka wa 1622 kipindi ambacho Papa Gregory XV alianzisha *Sacra Congregatio de Propaganda Fide* kwa maana ya mkusanyiko ulio takatifu kwa lengo la kueneza imani. Baada ya Papa kuona kuwa kulikuwa na vikwazo vingi katika kueneza imani, alianzisha kitengo cha Papa cha kueneza propaganda kama hatua ya kuwaunganisha wanawake na wanaume ‘kwa hiari’ ili waendeleze mafunzo ya kanisa. Kutokana na sababu hii, neno propaganda lilianza kuchukuliwa kama neno mbaya katika nchi za kiprotestanti. Wanaendelea kueleza kuwa neno hili limeibuka kutoka kwa ‘ushawishi’ na ‘maoni’ hadi kuwa uongo na udanganyifu.

Jowett na Donnell (2006) wanafafanua propaganda kama uendelezaji wa mawazo fulani. Wanaeleza visawe vya propaganda kama udanganyifu, uongo, upotoshaji, vita vya kisaikolojia na udhibiti wa akili. Ellul (1965) anafafanua dhana ya propaganda kama ushawishi wa kisaikolojia ulioratibiwa. Anaendelea kueleza kuwa propaganda hufanya kazi katika njia tofauti, ukweli nusu, ukweli kiasi na ukweli nje ya muktadha. Kwa mujibu wa Taylor (2003), propaganda ni mchakato wa kuanzisha na kukuza mawazo kwa namna fulani. Pia, ni mbinu za kimaksudi za kushawishi watu kufikiria na kutenda mambo kwa njia fulani inayohitajika. Ni kifaa kinachotumika na watu wanaotaka mamlaka au watu wanaotaka kuendelea kuwa na mamlaka. Taylor anahusisha propaganda na kitu kiovu kinacho chochea vita. Katika makala haya, utafiti utaonyesha uhusiano uliopo kati ya itikadi na propaganda kwa kujikita katika tamthilia teule za *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Kifo Kisimani*.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

## NADHARIA

Utafiti umeongozwa na nadharia ya Uchanganizi Tahakiki Usemi (UTU). Nadharia hii iliasisiwa na Fairclough Norman (1989) huko Lancaster School of Linguistics. Katika miaka ya 1970, nadharia ya UTU ilichimbuka kutokana na isimu jadilifu iliyoanzishwa katika Chuo Kikuu cha East Anglia. Waitifaki wa nadharia hii ni pamoja na Wodak (1997) na Dijk (1998). Dijk anajihusisha na nafasi ya mazungumzo katika uumbaji wa itikadi. Miriti (2016) anamnukuu Wodak (1997) kuwa UTU inahusika na kuangazia itikadi na utawala kutokana na data iliyozungumzwa, iliyoandikwa na inayoonekana. Anaendelea kueleza kuwa inaangalia lugha kama tendo la kijamii na kuona muktadha wa lugha kuwa muhimu sana.

Nadharia hii hueleza uhusiano uliopo kati ya matukio ya kiusemi, kisiasa, matini, kijamii na kiutamaduni inavyoathiriwa na itikadi. Na jinsi usemi huo unaathiri matukio katika jamii. Jelimo (2016) anaeleza kuwa nadharia hii inashughulikia masuala ya lugha na utamaduni wa jamii, inachunguza miktadha ya jamii kwa kutazama lugha kama uzoefu wa jamii. Kwa vile dhana za itikadi na propaganda zitabainishwa kutokana na matumizi ya lugha katika mazungumzo kati ya wahusika katika tamthilia teule, nadharia ya UTU inatufaa sana.

Fairclough (2001) anaeleza UTU kama sayansi muhimu sana ya kijamii inayoangazia matatizo ambayo watu wanakumbana nayo kutokana na hali fulani ya maisha katika jamii na jinsi ya kuepuka changamoto/matatizo hayo. Kutokana na Fairclough, dhana ya usemi huongozwa na itikadi. Kwa hivyo mtindo na mbinu ya uandishi huwa na athari za kiitikadi kwa vile huweza kuleta utofauti wa mahusiano kati ya wanajamii. Anaendelea kueleza kuwa uongozi wa sasa unafikiwa kutokana na itikadi zilizowekwa. Yaani, lugha ni zao la uhusiano baina ya utamaduni na muktadha.

Dijk (1993) anachukulia usemi kama tendo la kijamii. Anataja viwango viwili vya uchanganuzi wa usemi: Makro (inahusika na uongozi, utawala na unyanyasaji katika makundi ya kijamii) na Maikro (inahusisha matumizi ya lugha, usemi na mahusiano ya mazungumzo). Dijk (2001) anaeleza kuwa UTU hauhusishi tu maelezo na ufafanuzi wa usemi katika muktadha fulani bali pia unahusisha jinsi usemi unavyofanya kazi. Hasa majukumu ya usemi katika uzalishaji wa uongozi mbaya, kwa hivyo unaweka uhusiano kati ya lugha na utawala. Mihimili ya UTU itakayo ongoza utafiti katika makala haya ni; usemi, utamaduni, itikadi, muundo wa jamii na viwango vya uchanganuzi.

## MBINU ZA KUKUSANYA DATA

Utafiti huu ni wa maktabani. Watafiti walisoma tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Kifo Kisimani* zake Profesa Kithaka Wa Mberia. Pia, walisoma tasnifu na vitabu ambavyo vina ujumbe ambao unahusiana na mada. Watafiti walipekua makala ya mtandaoni pia kupata maarifa zaidi yanayohusiana na lengo la makala yanayotafitiwa. Utafiti huu umejikita katika muundo wa kimaelezo katika kubainisha na kufafanua ufungamano wa dhana za itikadi na propaganda katika tamthilia husika. Sampuli ambayo ni tamthilia teule imechaguliwa kimaksudi kwa sababu ina data inayohitajika. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Uhusiano Kati ya Itikadi na Propaganda katika Tamthilia Teule

Baadhi ya wataalamu kama vile Ellul (1965) wanaungama kuwa kuna uhusiano kati ya itikadi na propaganda. Wataalamu wengine hawajaungama wazi kuwa dhana hizi zina uhusiano, bali wameonyesha uhusiano wa dhana hizi katika ufafanuzi wa dhana za itikadi na propaganda. Kwa mfano, Jowett na Donell (2006) na Dijk (2006). Hoja zilizoelekeza watafiti kuonyesha uhusiano huu ni kuwa; diskozi huongozwa na itikadi, imani huendelezwa kwa kushawishi, propaganda huundwa kutokana na itikadi na fasili za dhana ya itikadi na propaganda.

#### *Diskozi Zote Huongozwa na Itikadi*

Kulingana na Dijk (2006), diskozi zote huongozwa na itikadi. Usemi unaotumika wakati wa mazungumzo huonyesha imani ya kundi hilo. Muhimili wa usemi unaotajwa na Dijk (1993) unatuelekeza katika kuonyesha uhusiano uliopo kati ya itikadi na propaganda. Usemi ni sehemu ya jamii kwa hivyo inaonyesha sifa, imani na maarifa ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

wahusika katika jamii. Kwa hivyo, usemi wowote ambao wahusika katika tamthilia teule wametumia unaongozwa na itikadi. Masuala ya kipropaganda yanayojitokeza katika usemi wao yanaongozwa na itikadi. Kwa kifupi, Dijk (2003) anaeleza kuwa itikadi hutoa maelekezo ya kila jambo linalotendeka katika jamii.

Gee (2015) anaeleza diskozi kama tabia, kuthaminiana, kuingiliana, kuaminiana, kufikiria, kuzungumza, kusoma na kuandika. Diskozi huendeleza kile ambacho kinatambulika kama kitambulisho cha jamii fulani. Imani ya jamii inatambulika kutokana na mazungumzo. Gee anaeleza mifumo mitano ya diskozi; namna maneno na sentensi za maandishi husemwa, namna sentensi huunganishwa na kuhusiana na sentensi nyingine, namna mazungumzo yamepangwa kwa jumla, uwekaji wa muktadha wa mazungumzo au maandishi na maudhui ya yanayozungumziwa. Mifumo hii huongozwa na itikadi. Itikadi huongoza muktadha wa mazungumzo na maudhui. Kwa hivyo, kuna uhusiano kati ya itikadi na propaganda kwa sababu itikadi na propaganda ni maudhui katika kazi za fasihi na huendelezwa kupitia kwa diskozi.

Kulingana na Kilimes na Marineli (2018), itikadi huongoza diskozi. Diskozi inayoendelezwa huwa na propaganda kama maudhui. Kwa hivyo, itikadi na propaganda hufanya kazi pamoja. Haya hudhihirika katika maudhui na muktadha wa mazungumzo kati wahusika. Naye Martin (2022) anaeleza kuwa itikadi huwa na seti za maarifa ambazo hulinda maslahi ya watu wa kundi fulani. Seti hizi hujitokeza katika diskozi kati ya wahusika. Diskozi huweza kuathiri diskozi nyingine kwa kupinga au kuunga mkono imani kati ya makundi mawili au zaidi. Propaganda huibuka wakati diskozi ya kundi moja inapinga au kukejeli imani ya kundi lingine. Kwa hivyo, itikadi huongoza diskozi zote.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, muktadha wa mazungumzo ya Gege na Mwelusi unaongozwa na itikadi ya ukombozi. Pavković (2005) anaeleza itikadi ya ukombozi ni seti ya imani, uamuzi wa thamani na maelekezo yanayoongoza hatua za kisiasa kwa lengo la kukomboa kundi linalokandamizwa. Usemi wa Mwelusi unashikilia kuwa Wanabutangi wanafaa kukombolewa na hivyo yeye na *Nuru ya Butangi* wana nia ya kufafanua misingi ya mashaka ya Butangi. Aidha, Gege anajaribu kushawishi Mwelusi dhidi ya imani yake ya ukombozi kwa kutumia usemi unaotaja chuki na fitina dhidi ya Bokono. Gege anaendeleza propaganda kwa kutumia semi za uongo ili kuchochea hisia za Mwelusi (Shabo, 2008). Hakuna ukweli uliodhibitishwa katika kauli yake kuwa Mwelusi anamchukia Mtukufu Bokono. Maongezi yao yanaongozwa na itikadi ya ukombozi. Mwelusi anaamini kuwa wataikomboa Butangi lakini usemi wa Gege unaoana na mawazo ya Gramsci na Bellamy (1994) kuwa ni vigumu kupata ukombozi (Uk. 45).

> ***"Mwelusi:** Chuki gani? Sisi akina nani?*
>
> ***Gege:** Samahani. Swali langu lina ncha mbili, kama upanga hatari! Ni nini kiini cha chuki yenu kali?*
>
> ***Mwelusi:** Unazungumzia nini, Gege?*
>
> ***Gege:** Tunazungumza. Mnachukia sana Mtukufu Mtemi Bokono; wewe na wengine wajiitao 'Nuru ya Butangi'*
>
> ***Mwelusi:** Hatuna chuki na Mtemi wala mtu mwingine yeyote.*
>
> ***Gege:** Usikane jambo wazi.*
>
> ***Mwelusi:** Hatumchuikii Mtemi.*
>
> ***Gege:** Basi kwa nini mnazurura kutoka sehemu moja ya Butangi hadi nyingine mkichochea fitina dhidi yake?*
>
> ***Mwelusi:** Tunafafanua msingi wa mashaka ya Butangi. Huko si kuchochea."*

Katika tamthilia ya M*aua kwenye Jua la Asubuhi*, muhimili wa usemi umetumika kubainisha uhusiano wa itikadi na propaganda kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Tungai, Kabitho na Waito. Usemi wao unaashiria imani yao kuhusu suala la ukombozi. Diskozi yao inaongozwa na itikadi ya ukombozi. Waito ana imani kuwa Wandiku wanaweza kukombolewa na kurudishiwa mashamba na ardhi zao zilizonyakuliwa kwa kuandamana au kushurutisha serikali kulinda haki zao. Imani ya Waito inaendana na mawazo ya Pavković (2005) ambayo yanashikilia kuwa, ili kujikomboa lazima nguvu na vurugu zitumike.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

Aidha, suala la propaganda linaendelezwa katika diskozi hii kwa sababu adui ambaye ni Watange amebainishwa (Shabo, 2008). Waito anashawishi mawazo na matendo ya Tungai na Kabitho kuwa wasiingie vitani bali wakabiliane na maadui wao kwa njia nyingine. Pia Kabitho anashawishi mawazo ya Waito anapomwonya dhidi ya kuambia mtu yeyote kuwa ameona bunduki pale. (Uk. 70).

> ***"Waito:*** *Moyo wangu! Nilikuwa mahali. Baada ya kusikia Habari nilizozisikia, moyo wangu uliniambia: 'Waito, kimbia! Kimbia ukazungumze na mjomba na shemegi. Usiwaache wamwage damu. Kimbia, Waito. Nenda ukawashawishi waache kuingia vitani' [Kimya kifupi]. Umri wangu ni mdogo kuliko wenu. Nakiri, kuishi kwingi ni kuona mengi. Kuishi kwingi kunaongeza mwangaza akilini. Lakini umri mdogo si ulemavu. Tafadhali. Nawaomba msifanye yale ambayo nimeyasikia.*
>
> ***Tungai:*** *Umesikia nini?*
>
> ***Waito:*** *Kwamba mnaunda kikosi cha kupigana vita na Watange. Tumetimuliwa kutoka mashamba yetu. Tumeuawa. Mali zetu zimeunguzwa……. lakini tusiingie vitani. Tukabiliane na wendawazimu wa Watange kwa njia tofauti*
>
> ***Kabitho:*** *Ondoka, Waito! Na usidhubutu kumwambia mtu yeyote kwamba umeona bunduki hapa.*
>
> ***Waito:*** *……Tutumieni mbinu tofauti kukomesha vitisho dhidi ya kabila letu.*
>
> ***Waito:*** *Zipo njia. Maandamano ya kila siku ni mojawapo ya njia.*
>
> *Kutokana na maelezo haya na diskozi kati ya wahusika ni dhahiri kuwa iwapo itikadi ya ukombozi haingekuwepo basi muktadha wa mazungumzo haya haungekuwepo. Propaganda imedhihirika kutokana na usemi wa wahusika ambapo diskozi yao imeelekezwa na itikadi ya ukombozi."*

### *Imani Huendelezwa kwa Kushawishi*

Kwa mujibu wa Dijk (1998), itikadi ni imani katika jamii kuhusu hali ya maisha inayojidhihirisha katika makundi fulani. Hakuna kundi ambalo linaweza kuendeleza imani yake bila kushawishi watu wa kundi hili au kundi lingine. Ushawishi huu ndio propaganda. Elull (1965) anaeleza propaganda kama ushawishi wa kisaikolojia ulioratibiwa. Kutokana na maelezo haya, ili imani iendelezwe kutoka kundi au kizazi kimoja hadi kingine, lazima ushawishi utumike.

Taylor (2003) anaeleza kuwa ili malengo ya kundi fulani yaafikiwe, lazima kuwe na wafuasi wapya. Pia wafuasi waliopo lazima washawishiwe kuendelea kuwa katika kundi hilo. Kundi la itikadi fulani lazima lipitishe ujumbe wake kwa kushawishi wanachama watarajiwa. Mafanikio ya kueneza itikadi hiyo hutegemea mbinu za ushawishi ambazo zinajikita katika hali ya mazingira inayowazunguka. Ushawishi huu ni uratibu wa mawazo ambao ni sifa ya propaganda. Kwa hivyo, propaganda ambayo ni ushawishi huendeleza itikadi.

Dhana za itikadi na propaganda ni tofauti lakini zina uhusiano; zinafanya kazi kwa pamoja. Propaganda inatumika kama mbinu ya kuendeleza imani ya kundi fulani. Kwa mfano, Fitzgerald (2011) anataja dini kama imani yenye sifa bia kuhusu uzoefu wa binadamu au taasisi. Kila dini hutumia ushawishi kwa waumini wake kuendelea kufuata itikadi zao. Ushawishi huu ni propaganda kwa sababu unaratibu watu kufikiria na kutenda mambo kwa njia fulani inayohitajika (Taylor, 2003). Itikadi ya dini inashawishi kundi lake kuwa Mungu ndiye hulipiza kisasi. Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi*, muhimili wa itikadi (Fairclough, 1989; Wodak, 1997) umetumika kutambulisha fikra za wahusika kuhusu dini. Dini imeshawishi mawazo yao kuwa hawafai kulipiza kisasi. Kwa mfano, dini ya Ukristo na Uislamu katika kitabu cha Warumi 12:9 na sura 16:126 mtawalia. Ushawishi huu ni propaganda; umetumiwa kuhakikisha kuna upendo, amani na kuzuia vurugu kama atajavyo Fitzgerald (2011). Kwa sababu ya kundi hili kushawishiwa, imekuwa vigumu kujikomboa kutoka katika hali duni ya maisha na uongozi mbaya. Wahusika wameshawishiwa na dini na wanaamini kuwa Mungu atawatoa kwenye mateso haya (Uk. 5).

> ***"Gachono:*** *[Huku ameelekeza mbinguni viganja vilivyofunuliwa] Ewe Mungu, Muumba wetu, mlizi wetu. Geuza sikio lako, ewe Mwenye-enzi, Ulielekeze kwenye kilio chetu.*
>
> ***Nyagachi****: Amina!*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

> ***Gachono:*** *Tazama nyuso zetu ambazo zimeloa machozi. Tuhurumie, ewe Mola*
>
> *Nyagachi: Amina!*
>
> ***Gachono:*** *Ewe Mungu, nyoyo zetu zinakulilia. Tuokoe kutoka kwenye mateso haya ili tuufurahie utukufu wako."*

Muhimili wa muundo wa kijamii (Fairclough, 1989) unaonyesha vikwazo vya kitabaka, cheo na hadhi vinavyopelekea kuwepo kwa semi zinazoashiria itikadi ya umwinyi. Kutokana na semi hizo, tunatambua namna wahusika wanashawishi wengine kuhusu imani ya umwinyi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa umwinyi ni mfumo wa kiuchumi ambao matajiri hurithishana utajiri huku wakimiliki mashamba makubwa pamoja na uwezo wa kisiasa. Watawala wanatumia nguvu kujirithisha mali na kupata mamlaka (Hilton, 1983).

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani,* Mtemi Bokono anashawishi Nyalwe kuamini kuwa ardhi ambayo Mgawa Ardhi alimpa Askari Mkuu si ya matumizi ya umma. Anaendeleza itikadi ya umwinyi kwa kushawishi mawazo ya Nywale kuwa anazijua kanuni za ardhi na kuwa hazikuwa zimevunjwa na mgawa ardhi. Bokono anaendeleza imani yake kwa kushawishi Nyalwe ambapo ushawishi huu ndio propaganda (Uk. 18- 19).

> ***"Nyalwe:*** *Ninayozungumzia ni muhimu. Usitie mzaha! Mama Agoro alikuja kulalamika. Anasema uwanja wa kuchezea Watoto wao umechukuliwa. Umepewa Askari Mkuu.*
>
> ***Bokono:*** *Aliyempa Askari Mkuu ni nani?*
>
> ***Nyalwe:*** *Mgawa Ardhi.*
>
> ***Bokono:*** *Basi kwa nini alikuja hapa badala ya kwenda kwa Mgawa Ardhi?*
>
> *uk 19*
>
> ***Nyalwe:*** *Kanuni zinazolinda ardhi ya umma.*
>
> ***Bokono:*** *Ingelikuwa ni ardhi ya matumizi ya umma, Mgawa Ardhi hangeitoa kwa Askari Mkuu.*
>
> ***Nyalwe:*** *Ni ardhi ya matumizi ya umma kwa mujibu wa kanuni za ardhi"*

Kutokana na maelezo na mifano mahususi katika tamthilia teule, ni wazi kuwa imani inaendelezwa kwa kushawishi kundi fulani. Ushawishi ni mojawapo ya sifa za propaganda. Kwa hivyo, propaganda hushawishi waumini ili kuendeleza itikadi fulani.

### *Propaganda Huundwa Kutokana na Itikadi*

Kwa mujibu wa Jowett na Donell (2012), itikadi huwa na elementi tano ambazo ni mitazamo, tabia, maadili, imani na utambuzi. Propaganda huundwa kutokana na elementi hizi. Iwapo jambo linaendelezwa kinyume na elementi hizi basi jambo hili ni la kipropaganda. Baadhi ya propaganda zinazotokana na itikadi ambazo utafiti utaangazia ni; propaganda inayotokana na itikadi ya utamaduni, propaganda inayotokana na itikadi ya dini na propaganda ya kijamii na kisiasa inayoendelezwa kutokana na itikadi ya umwinyi.

Ellul (1965), anaungama kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya itikadi na propaganda. Propaganda haikui kivyake bali huibuka itikadi inapojaribu kukua au kupanuka. Anaendelea kueleza kuwa propaganda hujipanga na kuendana na itikadi fulani. Aina za propaganda hutegemea itikadi ya wakati huo. Hutumia itikadi kwa lengo la kujihalalisha. Aidha, itikadi ambayo haitumiki katika propaganda haitiliwi maanani. Ellul anaendelea kueleza kuwa propaganda hutumia itikadi kwa lengo la kujihalalisha. Kulingana na Jowett na Donell (2006), mbinu zinazotumika kuendeleza propaganda ndizo aina za propaganda. Mbinu za propaganda hutambulika kutokana na muktadha wa mawasiliano, lengo la anayetuma ujumbe, ujumbe wenyewe na chombo ambacho kinatumika kutuma ujumbe na kuleta majibu ya ujumbe ule.

### Propaganda Inayotokana na Itikadi ya Utamaduni

Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla kulingana na Mbaabu (1985). Utamaduni wa jamii unaweza kujitokeza kutokana na usemi wa wahusika. Kama atajavyo Dijk (2001), kuna uhusiano wa karibu sana kati ya usemi, jamii na utamaduni. Kwa kuongozwa na muhimili wa utamaduni (Fairclough, 1989; Wodak, 1997), tutaweza kubaini itikadi ya utamaduni inayojitokeza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

katika usemi wa wahusika. Usemi huo utaonyesha propaganda inayotokana na itikadi ya utamaduni.

Utamaduni wa ukoo unaoletwa na ndoa umeendelezwa na mtunzi kutokana na usemi wa wahusika. Desturi ya mume kupeleka mali kwa familia ya mke kabla ya kuoana imedhihirishwa (Nsereko, 1975). Usemi ambao umetumika kudhihirisha utamaduni huu ni mahari, ndoa na harusi. Aidha, kutokana na usemi wa wahusika propaganda inajitokeza pia inayojihalalisha kutokana na itikadi ya utamaduni. Itikadi inaelekeza kuwa mume anafaa kujadili mahari, kulipa na kuoa. Watoto wanaopatikana wanakuza ukoo. Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi*, Kabitho anatumia imani ya utamaduni kushawishi mawazo ya Tungai ili ajiunge naye katika vita dhidi ya Watange. Anasihi Tungai kuwa ni zamu yake ya kumuunga mkono ili wafunze Watange adabu kwa sababu yeye alimuunga mkono wakati akimchumbia Wangane. Anatumia usemi kuwa 'uhusiano mwema ni wa nipe nikupe' unaoashiria propaganda kutokana na muktadha wa mazungumzo yao (Uk. 16-17).

> ***"Kabitho:*** *Ndugu yangu, wa tumbo moja, ndugu wa toka ni toke. Wangane ni nduguye Kabitho. Kimila, mtoto wa dada au kaka, au wa nduguye mtu, ni mtoto wa mtu huyo. Kwa hivyo Tungai, umeoa binti yangu. Ulipokuwa ukijadiliana mahari ya Wangane, ulikuwa ukiniona vikaoni. Nilikuwepo vikaoni kwa sababu mtoto wangu alikuwa anajiandaa kuondoka nyumbani mwangu. Siku ya arusi, uliniona katika kundi la wakwe wako. Sikukosa kuja kumuaga Wangane na kumpa baraka za safari njema ya ndoa. Mimi ni mkweo. Na ulipokuwa unataka kumwoa mtoto wangu sikukupiga breki. Nilikuunga mkono kikamilifu. Kweli au uwongo?*
>
> ***Toiche:*** *Ni kweli.*
>
> ***Kabitho****: Uhusiano mwema unajengeka katika "Nipe nikupe!" Sasa ni zamu yako ya kuniunga mkono. Hatuna budi kuwafunza Watange adabu na heshima."*

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, utamaduni wa ndoa unatumika kushawishi wahusika kutekeleza matendo ambayo yanafaidi watu wachache. Utamaduni unajitokeza kutokana na usemi wa Mweke anapomwahidi Gege kuozwa bintiye Mtemi. Anamwelezea alivyo na bahati kama ya mtende. Aidha, sauti i na ii ya Gege inaonyesha namna mawazo yake yalivyoshawishiwa kwa misingi ya imani ya ndoa. Anaiona ndoa hiyo kama lango lake la umaarufu. Pia, ni itikadi kuwa ndoa huunganisha watu. Itikadi hii inapelekea Gege kuwa na hamu ya kuozwa bintiye Mtemi ili awe na uhusiano na familia tajika. Utamaduni wa ndoa umehalalisha usahihi wa matamshi ya Mweke katika mawazo ya Gege na hivyo kupelekea Gege kutekeleza yale yote aliyoshawishiwa kuyatekeleza (Uk. 74-75).

> ***"Sauti i:*** *Mfunge Mwelusi kinywa upate Maisha mazuri.*
>
> ***Sauti ii:*** *La, Gege. Usimfunge nduguyo kinywa.*
>
> ***Sauti i:*** *Usikatae hurulaini kwa ajili ya kuogopa. Usiogope kashifa. Usikatae mali na umaarufu kwa ajili ya kuogopa kunyoshewa vidole. Kunyoshewa vidole si kufumwa kwa mishale. Ndiyo,Gege, ndoa na bintiye Mtemi ni lango la kuingia kwenye umaarufu. Usikatae kulipita. Ni ngazi ya kupanda angani. Usikatae kukanyaga vidato vyake. Ndoa Gege, ndoa, inakunyoshea mikono. Nyosha mikono yako uikaribishe! Karibisha maisha mapya, Gege!"*

## Propaganda Inayotokana na Itikadi ya Dini

Muhimili wa itikadi (Faiclough, 1989) unaeleza kuwa usemi unafanya kazi ya itikadi. Usemi wa wahusika unaonyesha itikadi yao kuhusu suala la dini. Itikadi ya dini inaelekeza kuwa uongozi hutoka kwa Mungu. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, itikadi ya dini inatumika kuendeleza propaganda chochezi. Mtemi Bokono anatumia itikadi ya dini kuchochea Zigu, Batu na Kame. Anatumia imani hii kusisitiza vitendo imara ambavyo vitakomesha wachochezi ambao wanazuia mpango wa Mungu wa kutaka Bokono aongoze kwa miaka mingi. Batu na Zigu wamehusishwa katika kuendeleza propaganda inayoendelezwa na Bokono. Wanatumia usemi kuwa Mungu aliyemketisha kitini angependa aendelee kuongoza Butangi kwa miaka mia moja. Hata hivyo, Bokono anashawishi mawazo yao kwa kuwaeleza kuwa ni jukumu lao kuamua iwapo Butangi itasonga mbele au itakwamishwa (Uk. 10).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

> ***"Bokono****: Uongozi hutoka kwa Mungu. Mamlaka yangu yametoka juu. Mungu akliniketisha kwenye kiti cha enzi cha Butangi. Alifanya hivyo kwa mapenzi yake kwa Butangi. Nia yake ni kuona kwamba Butangi inaongozwa kwa busara. Kwa hivyo, alinikweza kwenye kiti cha Mtemi.*
>
> ***Zigu:*** *Mungu mwenyewe alikuketisha kitini*
>
> ***Batu:*** *Na utaendelea kuongoza Butangi kwa manufaa ya Wanabutangi wote.*
>
> ***Zigu:*** *Utaongoza Butangi kwa miaka mia moja!*
>
> ***Bokono:*** *Nina hakika hivyo ndivyo angependa Mungu. Lakini ili hilo liwezekane, ni lazima uchochezi ukomeshwe. Na hiyo ni kazi yenu kama Baraza la Wazee. Amueni kama mnataka Butangi isonge iendelee kusonga mbele au ikwamishwe na uchochezi."*

Hapa, itikadi imeelekeza maadili na imani (Jowett & Donell, 2012) ya dini kuhusu chanzo cha mamlaka. Lakini, kutokana na muktadha wa mazungumzo ya wahusika, ni wazi kuwa wanaendeleza imani hii kinyume na imani inayokubalika. Dini haielekezi matumizi ya nguvu ili kuendelea kuwa na mamlaka. Mawazo yao ni ya kipropaganda. Wanatumia kama kifaa cha kuendelea kuwa na mamlaka (Taylor, 2003).

## Propaganda ya Kijamii na Kisiasa Inayotokana na Itikadi ya Umwinyi

Elull (1965) anaeleza kuwa propaganda ya kisiasa hushughulikia itikadi katika muktadha wa kijamii. Anaendelea kueleza kuwa aina hii ya propaganda hutumiwa na serikali au kundi fulani la watu kwa lengo la kubadili mawazo ya kundi lingine. Muhimili wa muundo wa kijamii (Fairclough, 1989) unaonyesha namna vikwazo vya kijamii vinaathiri usemi katika muktadha wa mazungumzo kati ya wahusika. Vikwazo vya kitabaka vimepelekea matabaka ya chini kudhulumiwa na matabaka haya yanapojaribu kujikomboa mawazo yao hushawishiwa na watawala ambao ni wa tabaka la juu.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, watawala wanatumia propaganda ya kijamii na kisiasa kuhalalisha matendo yao kwa kujikita katika itikadi ya umwinyi. Ni itikadi inayohusisha kurithishana mali, mashamba na uwezo wa kisiasa (Wamitila, 2003). Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Batu na Mwelusi, Batu ambaye ana uwezo wa kisiasa kutokana na mamlaka aliyopewa na Mtemi Bokono, anajaribu kushawishi mawazo ya Mwelusi. Anatumia itikadi ya umwinyi kujihalalisha. Anaendeleza imani ya kurithisha Mwelusi mamlaka, ardhi na ng'ombe ili kuratibu mawazo yake kwa malengo fiche. Uratibu huu ni propaganda (Uk. 31).

> ***"Batu:*** *Utatolewa humu hivi leo. Utapelekwa kwa mganga, utibiwe. Baadaye utapata chakula kizuri na malazi mema. Kesho asubuhi, watajie askari majina ya vijana wote wanaochochea chuki dhidi ya utawala wa Mtukufu Mtemi Bokono. Baada ya kufanya hivyo, mikutano itafanyika katika vijiji vyote vya Butangi. Utapelekwa katika kila Kijiji. Utawatangazia watu kwamba umeacha uchochezi baada ya kugundua kwamba uchochezi hauna manufaa yoyote. Pia utawaelezea umuhimu wa kuungana Pamoja chini ya uongozi wa hekima wa Mtukufu Mtemi Bokono. Nina hakika tunaelewana. Pia utawatangazia watu kwamba uchochezi katika Butangi umepangwa na majirani ambao wanaonea wivu amani na maendeleo yetu. Baada ya hayo, utafanywa kuwa kiongozi wa vijana. Utapewa ardhi nzuri na ng'ombe* idadi *utakayopendekeza. Utakuwa Tajiri kutajika ukiwa bado kijana."*

Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi*, kiongozi wa Watange ambaye ni Chebwe, anaendeleza propaganda ya kisiasa na kijamii kushawishi mawazo ya kundi la wapiganaji wakiongozwa na Toiche. Kutokana na muundo wa kijamii (Fairclough 1989), tabaka la chini limenyang'anywa ardhi lakini matabaka ya juu yana ardhi na majumba. Matabaka yamepelekea kundi la chini kutii na kufuata amri kutoka kwa tabaka la juu la watawala. Chebwe anaongozwa na itikadi ya umwinyi ya kurithisha watu ardhi ili kushawishi mawazo ya Toiche kutojiondoa kwenye kundi la wapiganaji. Anawaahidi wapiganaji kupewa ardhi yenye rotuba ambayo mito inapita katikati yake (Uk. 35).

> ***"Chebwe:*** *Huniamnini, Toiche?*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

> ***Toiche:*** *Naamini uamuzi wangu wa kutaka kujiondoa kundini.*
>
> ***Chebwe:*** *Baada ya kurejesha mashamba mikononi mwetu, wapiganaji watakuwa wa kwanza kupewa ardhi. Tutapata mashamba mengi yenye rotuba. Baadhi yake yana mito inayopitia katikati. Ukitaka kupewa mojawapo ya mashamba yenye mito nitahakikisha kuwa umelipata.*
>
> *Ili propaganda hii ifaulu au iwe sahihi mbele ya kundi linaloshawishiwa, imejikita katika itikadi ya umwinyi. Itikadi hii imetumika kuhalalisha propaganda ya kisiasa na kijamii."*

**Propaganda Inayotokana na Itikadi ya Ukombozi**

Montero (2009) anataja ukombozi kama mchakato unaohusisha mabadiliko ya kijamii kwa lengo la kuleta usawa, kupinga ukandamizaji na dhuluma pamoja na kuondoa taasisi zinazoyaendeleza maovu haya. Itikadi ya ukombozi hushawishi wanaokandamizwa kuhusu haki zao na manufaa ya kuishi katika jamii yenye demokrasia na usawa. Propaganda husishi hutumika na wanaoendeleza imani ya kupata ukombozi kufanya hadhira ya wanaokandamizwa kukubali kile wanachoambiwa bila kupinga lolote. Wanaokandamizwa wanashawishiwa kuamini kuwa wao ni wanyonge, wanakandamizwa na wanahitaji kujikomboa kutoka katika hali hii. Pasi kushawishiwa, ni vigumu kujihusisha katika mchakato wa kukombolewa.

Pavković (2005) anaeleza kuwa watesi hutumia ukatili na hivyo wanaodhulumiwa hutumia nguvu na vurugu ili kujiondoa katika ukatili wa watesi wao. Matumizi ya vurugu yanaashiria propaganda chochezi ambayo ina chembechembe za mapinduzi kama anavyotaja (Elull, 1965). Wanaodhulumiwa wanatolewa kutoka katika hisia za chuki hadi hisia za uasi. Aidha, kulingana na Gramsci na Bellamy (1994) ni vigumu kupata ukombozi. Wanaodhulumiwa wamezoea majukumu waliyopewa na watesi wao. Wanachukulia majukumu haya kuwa ya kawaida. Propaganda husishi imewafanya kuyakubali majukumu haya, mawazo yao yameratibiwa kuyakubali na hivyo ni vigumu kuwakomboa kutoka kwa watesi wao.

Kutokana na muhimili wa viwango vya uchanganuzi (Fairclough 1989), tunatambua muktadha wa mahusiano ya kijamii yanayoathiri usemi. Katika tamthilia *ya Kifo Kisimani*, mahusiano kati ya watesi na wanaodhulumiwa yanabainika wazi kutokana na usemi wa wahusika. Usemi wa wahusika kama vile Mwelusi na Azena unaashiria mani yao kuhusu ukombozi. Kwa upande mwingine usemi wa wahusika Bokono, Batu na Zigu unaashiria kuwa wao ni watesi na wanaendeleza uongozi mbaya. Mahusiano ya makundi haya mawili yanaashiria namna kundi ambalo linaongozwa na Mwelusi linavyojitahidi kujikomboa kutoka kwa uongozi mbaya wa Bokono na baraza lake. Katika uk wa 47, Mwelusi anatumia usemi kuwa anataka Butangi yenye haki, usawa na maendeleo. Anakemea watawala wanaopendelea baadhi ya Wanabutangi.

Azena anatumia usemi mabadiliko. Mabadiliko yanatokana na harakati za kupata ukombozi. Hii inaoana na propaganda chochezi ambayo vurugu hutumika ili waweze kujikomboa. Wanaodhulumiwa wanatumia mbinu chochezi kupata mabadiliko katika Butangi (Uk. 103).

> ***"Azena:*** *[kwa Bokono, akimwashiria Mweke kwa kidole] Samahani! Mmojawapo wa mikono mirefu ya Butangi umekwaruzwa kidogo. Mkono mrefu ulikuwa unataka kushambulia mabadiliko, mabadiliko yakaukwaruza kidogo."*

Muhimili wa usemi (Dijk 1993) unaonyesha imani inayoelekeza wahusika na jinsi imani hii inatekelezwa na propaganda. Katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi*, Waito anaamini kuwa ukombozi utapatikana kutokana na maandamano na kushurutisha serikali. Mawazo ya Waito yanaoana na yale Pavković (2005) kuwa ili watesi waweze kukombolewa, lazima nguvu na vurugu vitumike. Aidha licha ya kuelekeza wahusika kupata ukombozi, propaganda inatumika. Kabitho anashawishi Waito dhidi ya kutoelezea mtu yeyote kuhusu bunduki aliyoiona pale itakayotumika katika kukomboa Wandiku. Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati ya Kabitho, Waito na Tungai tunatambua propaganda chochezi katika usemi wao inayotekeleza itikadi ya ukombozi (Uk. 70-71). Waito anatumia semi za kuchochea zaidi hisia za Kabito na Tungai. Anawakumbusha jinsi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

walivyouawa, mali yao ilivyounguzwa na kuchukuliwa. Anasisitiza maandamano na kushurutisha serikali ili ilinde haki zao. Kwa hivyo, ili kupata ukombozi, lazima propaganda itumike kutekeleza mchakato huu.

**Propaganda Inayotokana na Itikadi ya Utawala**

Kulingana na Althusser (1981), itikadi ya kiutawala huendelezwa na sheria. Sheria na kanuni hutumiwa na watawala kuendelea kuwa na mamlaka wala si kulinda haki za wananchi wa kawaida. Hata hivyo, si watawala wote ambao wanatumia sheria kujifaidi bali utawala waweza kuwa na uongozi mzuri au mbaya kama wanavyotaja Mbatiah na Jagongo (2018). Utawala mzuri unahusisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma. Aidha, utawala mbaya unahusisha uongo, usiri, udanganyifu na upotoshaji katika kuendeleza uongozi. Sifa za uongo, udanganyifu na upotoshaji ni visawe vya propaganda kama wanavyobainisha Jowett na Donell (2006). Kwa hivyo, propaganda hutokana na itikadi ya utawala ili kuendeleza uongozi.

Tangus na Sang (2020) wanaeleza utawala kama mfumo unaofafanua mbinu zinazotumiwa na viongozi na mashirika. Mfumo huu huunda kanuni zinazostahili kulinda haki za binadamu na kuangazia sekta zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hata hivyo, watawala hutumia propaganda kushawishi wanajamii kufuata kanuni fulani zinazowakandamiza.

Usemi hutumika kuonyesha imani, sifa, maarifa na mahusiano baina ya watu. Muhimili wa usemi (Dijk, 1993) unaonyesha namna imani ya wanajamii inavyodhihirika kupitia kwa muktadha wa mazungumzo ya wahusika. Kuna uhusiano kati ya usemi na jamii, kwa hivyo usemi wa wahusika unaonyesha namna uongozi unavyoendelezwa katika jamii. Usemi unaashiria maudhui ya uongozi mbaya au uongozi mzuri. Itikadi ya utawala inaonyesha namna mawazo ya viongozi yalivyo mazuri kuhusu kanuni na sheria za kuwalinda wananchi lakini propaganda inaonyesha ni kwa namna gani mawazo haya yanayoonyeshwa ni mazuri. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, usemi wa wahusika kama vile Mtemi Bokono, Zigu, Batu na Kame unaashiria imani yao kuhusu utawala na namna wanavyotekeleza utawala wao (Uk. 65).

*“**Bokono:** Kumekuwa na maandamano tena? Wakazi wa Bulusi wameandamana tena?*

***Batu:** Hawatadhubutu tena, Mtukufu kiongozi mwema. Tatizo hilo nimelitatua kikamilifu. Hawataandamana tena……*

***Bokono:** Umefanya nini?*

***Batu:** Dawa ya moto ni moto. Askari waliwashambulia kwa moto.*

***Bokono:** Batu! Watu watasemaje kuhusu utawala wangu?*

***Batu:** Watawalaumu majirani. Kamwe hawatahusisha mkasa wao na utawala wa Butangi.*

***Bokono:** Sikubaliani na maoni yako.*

***Kame:** Hata mimi, mtukufu mtemi. Isitoshe, naona kama huo ni uovu usio na kifani.*

***Batu:** Uovu usio na kifani? Siasa haina uovu usio na kifani. Kuna mbinu tu. Mbinu za kuwanyamazisha wasioridhika.”*

Usemi wa Mtemi Bokono unaashiria namna anavyouenzi utawala wake. Kutokana na muktadha wa mazungumzo kati yake, Batu, Zigu na Kame. Wanaashiria uongozi mbaya. Baadhi ya semi wanazotaja ni; ‘*watalaumu majirani’*, ‘*siasa haina uovu’*, ‘*mbinu za kunyamazisha wasioridhika*’ na ‘*mbinu za kujikinga’*. Suala la kulaumu majirani wa Butangi ni la kipropaganda. Wanatumia propaganda ya siri kuendeleza utawala wao. Wakazi wa Bulusi hawana ufahamu kuhusu askari waliowashambulia kwa moto. Pia, propaganda chochezi imetumika na Batu kwa askari walio shambulia Bulusi baada ya wakazi hao kuandamana. Mbinu za kunyamazisha wasioridhika zinazotajwa na Batu ili kuendeleza itikadi ya utawala wa Bokono ni mbinu za kipropaganda ambazo zinazotumika na viongozi kwa manufaa yao ya kuendelea kuwa katika uongozi. Usemi kuwa ‘*usiponyoosha adui, atakunyoosha’* unaonyesha namna propaganda inatumika kuendeleza itikadi ya utawala ambayo inaendelezwa na matendo yanayoashiria uongozi mbaya.

Fairclough (1989) anataja muhimili wa itikadi kama mojawapo wa mihimili ya ya nadharia ya UTU.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

Kazi ya itikadi inaendelezwa na usemi ambao huonyesha namna watu wanaamini kuhusu watawala na utawala. Ni itikadi kuwa, kila jamii huongozwa na kanuni au sheria ambazo zimewekwa na watawala. Kanuni hizi zinaaminika kuwa nzuri na zina mipango mizuri kwa nchi. Lakini namna kanuni na sheria hizi zinatumiwa kudhibiti au kuwadhulumu wanaotawaliwa, mbinu za kipropaganda zinatumika. Propaganda inaonyesha ni kwa namna gani mawazo ya watawala kuhusu kanuni hizi ni mazuri au mabaya. Ni itikadi kuwa kila shirika huwa na kanuni zinazoiongoza. Kanuni za mashirika haya hujitokeza kwa usemi wa wanaohusika. Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, mtunzi ameonyesha kuwa kuna kanuni za gereza ambazo zinafaa kuzingatiwa. Aidha Askari II na Askari III wanaonyesha ni kwa namna gani kanuni hizi ni 'nzuri' ambalo ni suala la kipropaganda. Wanatumia kanuni za kiutawala kuwanyanyasa watu (Uk. 54).

> ***"Askari I:*** *Hebu kwanza simama kando mama. [Tanya anakwenda kando na kutua kikapu chake] Tumruhusu mama amwone mwanae!*
>
> ***Askari III:*** *Tukifanya hivyo tutakuwa tunavunja kanuni za gereza.*
>
> ***Askari II:*** *Ambalo ni jambo baya sana!*
>
> ***Askari I:*** *Kanuni zinazomzuia mzazi kumwona mtoto wake ni kanuni ambazo zimepita mipaka.!*
>
> ***Askari III:*** *Kanuni ni kanuni-ndani au nje ya mipaka!*
>
> ***Askari II:*** *Sioni kanuni za gereza zimepita mipaka vipi. Sioni vile kumzuia mharibifu kutangamana na watu wengine kunakuwa kanuni ambazo zimepita mipaka."*

## Fasili za Dhana ya Itikadi na Propaganda

Wataalamu mbalimbali wamefafanua dhana za itikadi na propaganda. Baadhi ya wataalamu ambao wamefafanua ya itikadi ni Eagleton (1991) na Larrain (1979). Eagleton anaeleza itikadi kama mawazo ya kundi fulani la kijamii au tabaka. Pia ni mawazo au fikra ambazo huhalalisha mamlaka ya kisiasa na seti za matendo zinazotekeleza vitendo. Larrain (1979) anaeleza kuwa Destutt de Tracy amebaini itikadi kama 'sayansi ya mawazo'. Anaendelea kueleza kuwa ni maoni ya fikra za wanadamu kuhusu wanayoyasema na wanayoyafikiria.

Kwa mujibu wa Taylor (2003), propaganda ni mchakato wa kuanzisha na kukuza mawazo kwa namna fulani. Maelezo haya yanashahibiana na yale ya Jowett na Donell (2006) kuwa propaganda ni uendelezaji wa mawazo fulani. Naye Bernays (2005) anafafanua propaganda kama jitihada thabiti za kudumu za kuunda matukio ya kushawishi mahusiano ya umma kwa kujikita katika mawazo fulani. Kulingana na Shabo (2008) propaganda ni ushawishi unaokusudia kuratibu mawazo na matendo ya watu wengine.

Kutokana na fasili za dhana ya itikadi na propaganda, ni dhahiri kuwa zote zinahusisha masuala ya mawazo ya watu. Itikadi ni mkusanyiko wa mawazo ambayo huratibiwa au kushawishiwa na propaganda. Kwa vile itikadi ni sayansi ya mawazo, mchakato wowote unaohusisha namna binadamu anavyofikiria na kusema ni wa kiitikadi kwa sababu watu husema na kutenda kile ambacho kipo katika mawazo yao. Kwa hivyo, propaganda na itikadi ni dhana mbili tofauti lakini zinahusiana sana. Itikadi huelekeza na propaganda hutenda mambo ambayo itikadi inaelekeza.

Katika tamthilia ya *Kifo Kisimani*, mawazo ya Mtemi Bokono yanabainika kutokana na mambo anayoyazungumza. Usemi (Dijk, 1993) kama muhimili wa nadharia ya Uchanganuzi Tahakiki Usemi unaonyesha imani, maarifa na mahusiano ya Bokono na wahusika wengine. Imani yake ni kuwa mamlaka yake ya kuongoza Butangi yanatoka kwa Mungu. Hapa, itikadi inaelekeza kuwa mamlaka yanatoka kwa Mungu lakini propaganda inatekeleza imani hii kwa kushawishi mawazo ya watu kuhusu uongozi huu. Bokono anatumia usemi unaochochea mawazo ya Zigu, Batu na Kame. Anasisitiza watumie vitendo kudhibiti wachochezi wanaojaribu kuzuia uongozi wa Mtemi uliotoka kwa Mungu (Uk. 10). Vitendo ambavyo anasisitiza vitumike ni propaganda. Vinatumika kutekeleza itikadi. Hata hivyo ili vitendo hivi (propaganda) vitekelezwe, lazima mawazo yahusishwe ambayo ni itikadi.

Kama anavyotaja Eagleton (1991), itikadi ni mawazo ya kundi fulani la kijamii au tabaka. Muhimili wa itikadi (Fairclough, 1989; Dijk, 2003) unaonyesha mawazo ya kundi la tabaka la chini la

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

kina Gachono na Nyagachi katika tamthilia ya *Maua kwenye Jua la Asubuhi*. Wanaongozwa na imani kuwa Mungu atasikia kilio chao na kuwa yeye ndiye tegemeo lao katika uk. 4-5. Hawataki kulipiza kisasi kama anavyopendekeza Kabitho. Mawazo yao yanadhihirika kutokana na muktadha wa mazungumzo yao. Badala ya kufanya wawezavyo kujiondoa katika hali ya mateso, wanaamini kuwa muumba na mlizi wao atawahurumia. Mawazo wanayoendeleza ni ya kipropaganda kama anavyotaja Jowett na Donell (2006) kuwa propaganda ni uendelezaji wa mawazo fulani ambayo yanahalalishwa na itikadi.

## HITIMISHO

Katika makala haya, watafiti wameonyesha kuwa itikadi na propaganda ni dhana ambazo zina uhusiano wa karibu sana. Baadhi ya wataalamu ambao wamedhihirisha haya katika maelezo yao ni pamoja na Ellul (1965), Jowett na Donell (2006) na Dijk (2006). Hoja ambazo zimetumika kuonyesha uhusiano huu ni pamoja na; diskozi huongozwa na itikadi, imani huendelezwa kwa kushawishi, propaganda huundwa kutokana na itikadi na fasili za dhana ya itikadi na propaganda.

Kwa kujikita katika tamthilia teule, imebainika kuwa diskozi zote huongozwa na itikadi fulani. Usemi unaotumika katika muktadha fulani wa mazungumzo huonyesha imani ya kundi hilo. Kwa hivyo, masuala ya kipropaganda yanayojitokeza katika usemi yanaongozwa na itikadi. Imani au itikadi huendelezwa kwa kushawishi watu katika jamii. Hakuna kundi ambalo linaweza kuendeleza imani yake bila kushawishi mawazo ya watu. Ushawishi huu ni propaganda. Pia, propaganda huundwa kutokana na itikadi fulani. Yani, propaganda huundwa ili iendane na elementi za itikadi ambazo ni mtazamo, maadili, imani na utambuzi. Mwisho, fasili za dhana ya itikadi na propaganda zinadhihirisha kuwa hizi ni dhana mbili tofauti lakini zinahusiana na kuingiliana. Dhana moja inatumika katika kuendeleza dhana nyingine. Itikadi inapoonyesha kuwa mawazo ya mtu ni mazuri, propaganda inaonyesha ni kwa namna gani mawazo haya ni mazuri.

## MAREJELEO


Althusser, L. (1981). Ideology and Ideological State Apparatuses. In Lenin and other Essays. (B.Brewster, mtaf). London. New Left Books.

Bernays, E. L. (2005). Propaganda. New York. Brooklyn Publishers.

Dijk, V. (1998). Ideology. A multidisciplinary Approach. London: Sage Publication.

Dijk, V. (1993). *Principles of Critical Discourse Analysis* in: Discourse and Society. London: Sage Publication.

Dijk, V. (2001). *Multidisciplinary CDA*: A Plea for Diversity in Ruth Wodak and Michael Meyer (eds) Methods of Critical Discourse Analysis, pp. 95–120. London: Sage.

Dijk, V. (2003). A Framework for Digital Divide Research. Electronic Journal of Communication Vol 12 Number 1,2 (2002).

Eagleton, T. (1991). *Ideology:* An introduction. London: Verso.

Ellul, J. (1965). *Propaganda: The Formation of Mens Attitudes*. New York. Vintage Books.

Fairclough, N. (1989). *Languange and Power*. London. Longman Publishers.

Fairclough, N. (2001). Language and Power (2nd ed.). New York. Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315838250. Accessed on 12th March 2022.

Fitzgerald, T. (2011). Religion and Politics in International Relations: The Modern Myth. London: Bloomsbury.

Gee, J. P. (2015). Social linguistics and Literacies; Ideiology in Discourse 5th Edition. New York. Routledge Publishers.

Gramsci, A. (1971). *Selections from the Prison Notbooks of Antonio Gramsci*. New York: International Publishers.

Gramsci, A, & Bellamy. R. (ed). (1994). Pre-Prison Writings. London. Cambridge University Press.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

Hilton, R. (1983), Feudal society in T BOTTOMORE et, al. Dictionary of Marxist Thought.

Oxord. Blackwell company.

Jelimo, D. (2016). Matumizi ya mbinu za ufupishaji katika mitandao ya kijamii na athari zake katika lugha ya Kiswahili. Tasnifu. Kenyatta University.

Jowett, G. S., & Donell, V. (2006). *Propaganda and Persution*. London. Sage Publications Ltd.

Kilimes, O., & Marineli. M. (2018). Introduction: propaganda and political Discourse in the Xi Jinping Era. Journal of China Political Science. Vol 23, pp 313-322. July 2018. hhttps://doi.org/10.1007/11366-018-9566-3 accessed on 19th July 2022.

Kithaka wa Mberia. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi. Marimba Publications.

Kithaka wa Mberia. (2004). *Maua kwenye Jua la Asubuhi*. Nairobi. Marimba Publications.

Kitto, I .B. (2019). *Kuchunguza Siasa na Itikadi katika Tamthilia ya Nyota ya Mboya*. Shahada ya uzamili Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.

Larrain, J. (1979). *The Concept of Ideology*. London. Hutchinson &Co. Publications Ltd.

Marx, K., & Engels, F. (1977). The German Ideology. London: Lawrence and Wishart.

Martin, C. (2022). Discourse and ideology. A critique of the study of culture. New York. Bloomsbury Publishers.

Mbaabu, I. (1985). Utamaduni wa Waswahili: Kenya publishing and Book Marketing C.O ltd.

Mbatiah. J., & Jagongo. A. (2018). Good Governance, Development Expenditure and Economic Growth: Theoretical Review. International Journal of Management and Commerce Innovations ISSN 2348-7585 (Online) Vol. 5, Issue 2, pp: (802-809), Month: October 2017 - March 2018.

Mlaga, W. (2020). *Uhusiano wa Propaganda na Fasihi*: fasili Maendeleo na mdhihiriko wake. MULIKA Na 38. Chuo kikuu cha Rwanda.

Miriti, M. K. (2016). *Figurative Language in Electoral Campaign Speeches*: A Critical Discourse Analysis Approach. M.A Thesis. Kenyatta University.

Montero, M. (2009). Methods for Liberation: Critical Consciousness in Action. In: Sonn, C., Montero, M. (eds) Psychology of Liberation. Peace Psychology Book Series. Springer, New York, NY. https://doi.org/10.1007/978-0-387-85784-8_4

Murithi, J. (2017). *Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.* Tasnifu Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nsereko, D. D. (1975). The Nature and Function of Marriage Gifts in Customary African Marriages. *The American Journal of Comparative Law*, *23*(4), 682–704. https://doi.org/10.2307/839241

Pavković, A. (2005). Terrorism as an instrument of liberation: a liberation ideology perspective. In G. Meggle (Ed.), *Ethics of terrorism and counter-terrorism* (pp. 245-260). (Philosophical research). Ontos Verlag. https://doi.org/10.1515/9783110327496.253

Prantkanis, A. & Aronson, E. (2001), Age of Propaganda: The everyday use and abuse of persuation. Santa Cruz. University of California.

Shabo. M. E (2008). Techniques of Propaganda and Persuation. U.S.A. Prestwick House, Inc.

Tangus. C, & Sang. P. (2020). Linking Governance to Performance of Government-funded Projects in Kenya. THE INTERNATIONAL JOURNAL OF BUSINESS & MANAGEMENT. Vol 8 Issue 11. November, 2020

Taylor, P. M. (2003). Munitions of the mind: A History of Propaganda from the Ancient World to the Present Era. Manchester & New York: Manchester University Press.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1004

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya fasihi: istilahi na nadharia. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wodak, R. (1997). Gender and Discourse. London: Sage Publications.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.